**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA**
**MITAAHALMASHAURI YA MANISPAA YA**
**UBUNGO**

**SHULE YA SEKONDARI MATOSA**
**SIMU**
**0655364331**
**0713242395**
**0754364331**

**S.L.P 55107**
**DAR ES SALAAM**

**Matosasec2009@yahoo.com**

---

**JINA LA MWANAFUNZI ..........................................................................**

**FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA-2023**

Uongozi wa shule ya Sekondari Matosa unayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiungakidato cha kwanza mwaka 2023, ukiwa mwanafunzi wa kutwa. Hongera sana kwa
kupata nafasi hii adimu. Vipaumbele vyetu ni: Nidhamu, Taaluma, Uzalendo na Uwajibikajimakini.

**MAHALI SHULE ILIPO:**

Shule hii ipo mkoa wa Dar es Salaam wilaya ya Ubungo, kata ya Goba, mtaa wa Matosa. Umbali kutoka Kimara mwisho ( barabara ya Morogoro) kufika shuleni ni kilomita 6.

**MUDA WA KUFUNGUA SHULE:**

shule itafunguliwa tarehe 09/ Januari/ 2023 saa moja kamili (1:00) asubuhi fika na vitu vyotevinavyohitajika ili uweze kusajiliwa. Mwanafunzi ambaye hataripoti kwa muda uliopangwa,nafasi yake itajazwa na mwanafunzi mwingine.

**MAHITAJI MUHIMU YA KUJA NAYO SHULENI**

1. Sare ya shule.
2. Begi la shule la kubebea madaftari.
3. Rim moja kwa mwaka (**aina ya multifunctioin NO.1**)
4. Mkebe wa vifaa vya hisabati.
5. Madaftari 11 counter book ( quire 3 au 4)
6. Kamusi (dictionary) English to Kiswahili au English to English.
7. Mathematical four figure table.
8. Kalamu za wino na risasi pamoja na rula.
9. Truck Suit rangi ya …………………..
10. Faili la mwanafunzi ( flat file)
11. Sweta la mikono mirefu rangi ya kijani (suruali au sketi ya shule)
12. Kwa wanafunzi wanaojiunga na kidato cha kwanza wanatakiwa watengeneze ufagio wachelewa waje nao na utakaguliwa siku ya kuwasili shuleni.

**MAELEZO YA SARE YA SHULE:**

**WAVULANA:**

- Shati jeupe la mikono mifupi lisilo bana – pea mbili.
- Suruali rangi ya kijani yenye upana wa cm 17/18 chini na marinda mawili kila upande pea mbili ( kijani namba 1)
- Soksi rangi nyeupe pea mbili (ndefu)
- Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na kisigino vya kufunga kwa kamba.
- Nywele fupi sio kipara.
- Mkanda mweusi wa ngozi.

**WASICHANA:**

- Shati jeupe la mikono mifupi lisilo bana – pea mbili.
- Sketi rangi ya kijani ya jeshi mamba - 1, mshono wa marida box pea mbili.
- Soksi rangi nyeupe pea mbili (ndefu)
- Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na kisigino vya kufunga na kamba.
- Nywele fupi sio kipara.
- Wanaovaa hijabu sketi iwe ndefu mpaka kwenye kifundo cha mguu.
- Nusu kanzu ivuke kiuno na isibane kuonyesha mwili.
- Juba mpaka tumboni.

**SHERIA ZA SHULE:**

**Nidhamu kwa ujumla:**

1. Ni lazima mwanafunzi awahi shuleni asubuhi saa 12:45na kufanya usafi wa mazingira ya shule pia kuhudhuria gwaride la ukaguzi wa usafi wa kuchangamsha mwili.
2. Mwanafunzi yeyote hawaruhusiwi kuondoka katika eneo la shule bila kupata kibali cha maandishi kutoka kwa mwalimu wa darasa, wa zamu, idara ya nidhamu, malezi au mkuu wa shule.
3. Mwanafunzi anatakiwa kusimama, kusalimia na kuwapokea mzigo walimu au mtu yeyote mwenye umri mkubwa Zaidi yake popote pale akutanapo na watu wa aina hiyo.
4. Hairuhusiwi kutumia LUGHA CHAFU miongoni mwa wanafunzi na kwa mtu mwingine yeyote.
5. Mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu wanafunzi wenzake, viranja na wafanyakazi wote wa shule.
6. Kila mwanafunzi lazima ahudhurie vipinid vyote vya darasani na shughuli za michezo, na uzalishaji mali kwa mujibu wa ratiba.
7. Mwanafunzi lazima afanye mitihani ya masomo yite anayososma shuleni.
8. Mwanafunzi awapo shuleni haruhusiwi kuwa na aina yeyote ya vitu vifuatavyo: kucha ndefu, kupaka rani, kuvaa cheni, kuvaa hereni, nyele ndefu, kunyoa kipara, kunyoa nyusi, kupaka dawa nywele, kupaka ina, kuchora tatuu, n.k.
9. Mwanafunzi ahakikishe kuwa awapo mahali popote ndani au nje ya shule awe amevaa nguo za heshima. Ni marufuku kuvaa nguo zinazobana, fupi na nyepesi.
10. Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo Zaidi ya zile zilizotajwa katika maelekezo ya kujiunga na shule, ikiwemo sweta la rangi inayotakiwa.

11. Wanafunzi wanatakiwa kutunza mali zao binafsi na mali za shule. Pia wanatakiwa kutoa taarifa kwenye utawala juu ya uharibifu wa mali ya shule.
12. Ni marufuku kwa mwanfunzi kwenda kwenye maeneo yafuatayo bila sababu maalum au bila kupewa ruhusa:-
    i. Shule za jirani na madukani
    ii. Nyumba zinazozunguka shule
    iii. Vibanda vya biashara nje ya shule
    iv. Nyumba au makazi ya walimu.
13. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuklutwa sehemu zifuatazo:-
    i. Baa na klab za usiku
    ii. Nyumba za kulala wageni isipokuwa wanapokuwa na wazazi au walezi wao.
    iii. Fukwe za bahari (beach) isipokuwa kwa idhini ya uongozi wa shule.
14. Wawapo shuleni wanafunzi hawaruhusiwi kumiliki vitu vya gharama kama simu ya mkononi, redio, kamera, ipad, albam za picha na CD, vocha na laini za simu.
15. Kila mwanafunzi ni lazima afanye bidi katika kila somo. Mwanafunzi ambaye atapata chini ya 50% mwisho wa mwaka atakariri darasa (atarudia)
16. Hakikisha ukimya au utulivu wa hali ya juu unazingatiwa katika maeneo ya shule nay a kujifunzia has darasani, maktaba, maabara na koridos wakati wa vipindi.
17. Adhabu ya viboko itaruhusiwa kwa kosa linalostahili na kuwa na taarifa/ kibali cha mkuu wa shule.
18. Hakikisha muda wote unapokuwa shuleni unaongea lugha ya kiingereza nje na ndani ya darasa.
19. Mwanafunzi yeyote akikamatwa na kitu chochote kisichotakiwa shuleni kitahariwa mbele yake.

**MAKOSA AMBAYO MWANAFUNZI AKIYAFANYA ANWEZA KUFUKUZWA SHULE**

1. Kutokuchukua ripoti ya maendeleo yake ya nusu mwaka au mwaka.
2. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
3. Aina zote za wizi na unyang’anyi.
4. Aina zote za makossa ya kujamiana na uasherati. Hii ni pamoja na kukutwa na mikanda ya video, vitabu vichafu vya uasherati au vitu vinavyofanana na hivyo.
5. Kupiga au kupigana
6. Matumizi ya lugha chafu au matusi
7. Makossa ya jinai
8. Kuzomea watumishi au kuchokoza wanafunzi wengine.
9. Kugoma au kuchochea mgomo (ghasia)
10. Kutohudhuria shuleni kwa muda wa siku 30 mfululizo.
11. Kudharau bendera ya Taifa kwa kutokuhudhuria paredi.
12. Kupara mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule, (pia ikidhibitika kutoa mimba)
13. Kuoa au kuolewa.
14. Kukuwadia au kushawishi wanafunzi wenzie na mtumishi yeyote katika mambo ya mapenzi ndani na nje ya shule.
15. Kunyanyasa mwanafunzi mwenzie kutokana na jinsia yake, udini, ulemavu, ugeni wake au hali yake.
16. Kughushi mitihani au wizi wa mitihani, kukataa au kutokufanya mitihani, majaribio, mazoezi ya masomo bila sababu za msingi.
17. Kukataa adhabu kwa makusudi. Pia adhabu inaweza kutolewa na mwalimu au kireanja yeyote kwa mwanafunzi anayeonyesha utovu wa nidhamu.

18. Kuharibu mali ya shule ikiwa ni pamoja na majengo, mabomba ya maji, mali ya mtu au kundi la watu.
19. Kukamatwa na simu, redio, kamera, ipad, albamu na CD kwa mara ya pili baada ya kuonywa kwa mara ya kwanza.
20. Kucheza Kamari, pray station (PS), kucheza pull table nk.

**WAJIBU WA MZAZI**

1. Mzazi/ mlezi anatakiwa kumleta mwanae kumwandikisha shuleni anapoanza masomo.
2. Mzazi/ mlezi anatakiwa kuandikisha majina ya watu wane na namba zao za simu watakaoruhusiwa kupata ripoti za mtoto akiwa shuleni na mawasiliano ya vikao, wito. N.k.
3. Mzazi/ mlezi anatakiwa kuja kuchukua ripoti ya mtoto wake kwa muhula husika vinginevyo hatapokelewa muhula unaofuata.
4. Mzazi/ mlezi anatakiwa kuja shuleni kwa muda muafaka pindi anapohitajika na uongozi wa shule.
5. Mzazi/ mlezi ajenge tabia ya kutembelea shule mara kwa mara ili kujua maendeleo ya mtoto wake ili kujenga mshikamano wa malezi. ( kila mwezi mzazi afike bila kuitwa)
6. Mzazi/ mlezi amfahamu kwa jina na namba ya simu ya mwalimu wa darasa la mtoto wake ili kujenga mahusiano ya malezi ya mtoto.
7. Mzazi ahakikishe amempima afya mtoto wake kisha alete ripoti ya daktari na kama anamatatizo ya kiafya alete vithibitisho ili kuepusha mtoto kupewa adhabu itakayomuumiza.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YETU.**

**……………………………………………..**

**Mwl. Bundala Elias Masanyiwa**
**MKUU WA SHULE**

## KIAMBATANISHO 'A'
## FOMU RASMI YA KUANDIKISHWA

PICHA

Sehemu hii ijazwe na mwanafunzi:-

1. Jina kamili la mwanafunzi
   ………………………………………………………………………
2. Uraia
   …………………………………………………………………………………………….
3. Dini
   ……………………………………………………………………………………………
4. Tarehe ya kuzaliwa
   ……………………………………………………………………………….
5. Mahali alipozaliwa
   ……………………………………………………………………………..
6. Yatima/ sio yatima/mzazi mmoja (kata isiyohusika)
7. Shule aliyosoma kabla ya kuja sekondari ya.................................................(jaza jedwali)

| JINA LILILOANDIKISHWA SHULENI | SHULE YA MSINGI ALIPOTOKA | MWAKA ULIOANZIA | MWAKA ULIOTOKA |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |

Saini ya mwanafunzi ..........................................................................................Tarehe ……………..……

PICHA

**Sehemu hii ijazwe na mzazi/ mlezi**

1. Jina kamili la mzazi/ mlezi……………………………………………Uraia……………………
2. Anuani kamili mjini DSM …………………………………………………….
3. Sehemu anayoishi wilaya……………………………………………………………………….
4. Mtaa………………………Kata…………………………………………………………………….
5. Namba ya simu…..........................................................................................(ya haraka)

Maelezo ya kikazi ya msaidizi/ mlezi:

1. Jina la mwajiri na idara……………………………………………………………………..
2. Anuani………………………………….Namba ya simu……………………………………….
3. Kazi ya mzazi/Mlezi……………………………………………………………………………….
   (mfano: karani,mwalimu, mfanya biashara n..k)

Saini ya mzazi/ Mlezi……………………..Tarehe……………………………………

(mawasiliano ya ndugu wa karibu)

1. Jina ……………………………………………… Simu ………………………………………
2. Jina ……………………………………………… Simu ………………………………………
3. Jina ……………………………………………… Simu ………………………………………
4.

## KIAMBATANISHO "B"
## AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi ……………………………………………………………………………………………

1. Nimeyasoma na kuyaelewa maelezo yote na nimekubali kujiunga na shule ya sekondari ……………………………… kuanzia tarehe …………………………
2. Naahidi kwamba;-
   a) Nitazingatia sheria zote za shule na kutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa.
   b) Sitashiriki katika vitendo vya hujuma wala vitendo ambavyo vitakua kinyume na serikali ya jamhuri ya muungano wa Tanzania.
   c) Nitatunza mali ya umma ambayo ni pamoja na majengo, samani, vitabu na na vifaa vya maabara.
   d) Nipo tayari kuchukuliwa hatua yoyote stahiki endapo nitakiuka maelekezo yaliyotolewa kwenye fomu hii.

Saini ya mwanafunzi .................................................................... Tarehe …………………………….

---

## AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi mzazi/mlezi wa ………………………………………………… kidato cha ……………
Naahidi kwamba;-

a) Nitashirikiana kikamilifu na uongozi wa shule na walimu wote kwa ujumla katika kumuelimisha na kumlea mtoto wangu. Hii ni kuhakikisha kuwa atazitii sharia zote za shule na kuyazingatia mambo yote muhimu yaliyotajwa.
b) Nitafanya kila niwezalo kumwezesha mwanangu kufika shule kila siku kabla ya saa 12:45 asubuhi.
c) Na kwamba mwanafunzi atahitimu na kufuzu kidato cha kwanza hadi cha nne.
d) Ninaruhusu mwanangu achukuliwe hatua yoyote stahiki endapo **ATAKIUKA** mojawapo ya sharia na kanuni zilizoorodheshwa.

Saini ya mzazi/mlezi ....................................................................... Tarehe …………………………….

## KITABULISHO "C"
## FOMU YA MAOMBI YA KUPIMWA NA DAKTARI

**Nenda na fomu hii kwa mganga au daktari akupime na kukujazia fomu hii ipasavyo.**
**(Upimaji huu ni lazima ufanyike katika zahanati au hospitali ya serikali)**

**SHULE YA SEKONDARI MATOSA,**
**S.L.P 55107**
**DAR ES SALAAM**
**TAREHE ……………………….**

**Mganga mkuu wa mkoa/wilaya/kituo cha afya**
**S.L.P ………………..**
**……………………………………..**

**<u>MEDICAL CERTIFICATE:</u>**

1. **Jina la mwanafunzi ………………………………………………………………**
2. **Kidato cha …………………………………….**
3. **Nimempima mtajwa hapo juu na kumwona amepatikana/hakupatikana na ugonjwa wa ......................................................................................Na kutibiwa ipasavyo.**
4. **Nimempima mtajwa na kumuona anaweza/hawezi kuendelea na masomo kwa sababu ……………………………………………………………………………………… …………………**
5. **(KWA MSICHANA TU) Nimemwona hana/ana mimba ya miezi ……………………………………….**

***Tutakaowatilia mashaka tutawapeleka kwa daktari***

6. **AFYA KWA UJUMLA**
   a) **Kifuakikuu ………………………………………………………………………**
   b) **Macho ……………………………………………………………………………**
   c) **Masikio …………………………………………………………………….......**
   d) **Akili ……………………………………………………………………………..**
   e) **Kilema chochote ……………………………………………………………**
   f) **Mkojo ……………………………………………………………………………**
   g) **Choo(stool) ……………………………………………………………………….**
   h) **Mengineyo (YATAJWE) ………………………………………………………**

**Jina la daktari ………………………………………………………………………**

**Sahihi ………………….... Cheo..........................................................Mhuri …………………………….**